



## Maombi huleta mabadiliko. Mungu hufurahia watoto wanapoomba.

“wakamwambia wasikia hawa wasemavyo,” Yesu akajibu akawambia, “kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa?”  
*Matthew 21:16*

Kuna changamoto kadha wa kadha zinazowakabili watoto na vijana wa kati hasa katika miji mikubwa ya nchi zinazoendelea, matatizo ambayo yanawanyima fursa ya usalama na kupendwa ndani ya familia kama Mungu alivyokusudia. Katika maadhimisho ya 21 ya wiki ya maombi kwa watoto Duniani wajibu wetu ni kuhamasisha mamilioni ya watoto duniani kuomba ili wawe na maisha salama.

### JIUNGE NASI KATIKA MAOMBI...

Bwana Yesu,  
Tusaidie wote kuwafundisha, kuwajengea uwezo watoto kuwa waombaji.  
Tupe uwezo na nguvu ya kuomba maombi yenye kubariki watoto wa kizazi hiki.  
Pia tunaomba kupitia maombi haya uwaguse na ujibu mahitaji magumu ya yatima ili iwe sababu ya wao kusogea karibu zaidi na wewe.  
Bwana tufundishe namna ya kuomba. Amen

## SABABU 10 ZA KUWA NA WIKI YA MAOMBI KWA WATOTO

### 1 Chimbuko

Maombi ndiyo chimbuko la kuanza kwa VIVA miaka 21 iliyopita.

### 2 UMOJA

Tukiomba kwa pamoja, tunapata matokeo

### 3 Utu

Huimalisha utu wetu.

### 4 Mwelekeo

Inatupa kujua mambo mengi kuhusiana na watoto walio katika mazingira magumu.

### 5 Hatua

Inatuongezea nguvu ya kutimiza lengo letu la kuwasaidia watoto.

### 6. Urahisi

Hufanya mambo magumu yawe rahisi.

### 7 Baraka

Watu hujitoa na Mungu anawabariki.

### 8 Ushirika

Maombi hupanua mtandao na ushirikiano.

### 9 Kujenga uwezo

Maombi huwajengea uwezo watoto wa kuongoza

10. Kuimalishwa – Maombi hutuimalisha

## Vifungu vya msingi

Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia Bwana, tufundishe kusali kama Yohana alivyowafundisha watu wake. *Luka 11:1*

Vinywani mwa watoto wachanga umeiweka misingi ya nguvu kwasababu yao wanaoshindana nawe uwakomeshe adui na majilipiza kisasi. *Psalm 8:2.*

Usiseme maneno ya ujinga kwa kinywa chako ,wala moyo wako usiwe na haraka kunena mbele za Mungu kwa maana mungu yuko juu nawewe uko chini, kwa hiyo maneno yako na yawe machache . *Mhubiri 5:2*

Akapewa uvumba mwingi ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote. *Ufunuo 8: 3b, 4*

Bwana akaja, akasimama, akaita vilevile kama kwanza Samweli, Samweli, Ndipo Samweli akasema nena Bwana kwa kuwa mtumishi wako anasikia.”  
*1 Samuel 3:10*

Basi wewe usalipo ,ingia katika chumba chako cha ndani na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini na Baba aonaye sirini atakujaza.  
*Matayo 6: 6*

## Mambo unayoweza kufanya katika wiki ya maombi

**Mifano ya shughuli zilizotekelezwa katika wiki ya maombi katika nchi mbalimbali.**

**Italy:** Wiki ya maombi ilihusisha michezo mbalimbali, mashairi, maigizo, nyimbo na kufanya maandamano ya amani mjini.

**Oxford, UK:** Ibada ya jioni ya maombi ilifanyika chini ya usimamizi wa mashirika kadhaa katika Syria/Lebanon, Gaza/Palestine ikihusisha watoto wa wanajeshi. Waliweza kuangalia video za za kutafakarisha..

**Kansas, USA:** Watoto 100 kuanzia chekechea hadi darasa la 8 walishiriki na kuongoza wao wenyewe maombi na walitoa ujumbe .

**Mwanza, Tanzania:** Watoto waliomba siku hiyo , pia watoto walipata fursa ya kula, kuimba na kuigiza .

**Guduru, India:** Yalifanyika Maombi, mradi ulitembelea vituo vya yatima. Na pia kukusanya michango toka kwa washirika kwa ajili ya fedha zaidi za kusaidia watoto wengi zaidi.

**Wan Chai, Hong Kong:** Maombi kwa waumini wote na kutoa ujumbe wa kuwahusu watoto kwa kanisa lote kupitia mtandao wa viva.

**Zimbabwe, Harare:** Watoto waliomba nyumbani pamoja na baadaye walikusanyika jumapili kanisani kwa maombi..

**Tembelea tovuti, [www.worldweekendofprayer.com](http://www.worldweekendofprayer.com) kwa taarifa nyinginezo zikiwemo**

- Mafunzo ya namna ya kufundisha watoto kuomba.
- Vitabu vinavyotoa mwongozo kuhusu maombi ikiwemo na habari ya Hanna.
- Sehemu ambayo watoto wanaweza kutuma picha za matukio ya wiki ya maombi.

Wiki ya maombi ni wiki ya kimataifa inayojumuisha watu wazima na watoto katika kila juma la kwanza la mwezi Juni ambao maelfu ya watu kutoka zaidi ya nchi 40 hujumuika.

Viva ni shirika la kimataifa la kikiristo linawafikia watoto kwa nguvu ya pamoja ya umoja wa kimtandao kupitia mashirika toka nchi 37 za jamii tofautitofauti duniani.